JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA
ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001: 2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

MACHI 2024

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA
ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001: 2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

MACHI 2024

# YALIYOMO


**NENO LA MWENYEKITI WA BODI** ..... iii
**DIBAJI** ..... iv
**VIFUPISHO VYA MANENO** ..... vi
**VIPIMO NA ALAMA** ..... vi
**FASILI YA VIASHIRIA VIKUU VYA UTENDAJI** ..... vii

**SEHEMU YA KWANZA** ..... 1
**1.0 UTANGULIZI** ..... 1
1.1 Majukumu ya EWURA katika Sekta ya Maji ..... 1
1.2 Dira ya EWURA ..... 2
1.3 Dhamira ya EWURA ..... 2
1.4 Lengo la Taarifa ..... 2
1.5 Maelezo kuhusu Mamlaka za Maji ..... 3
1.6 Mbinu za Uandaaji wa Taarifa ..... 5

**SEHEMU YA PILI** ..... 6
**2.0 UCHAMBUZI WA UTENDAJI** ..... 6
2.1 Uzalishaji na Mahitaji ya Maji ..... 6
2.2 Kiwango cha Upatikanaji wa Maji ..... 6
2.3 Kiwango cha Ubora wa Maji ..... 7
2.4 Upatikanaji wa Huduma za Usafi wa Mazingira ..... 8
2.5 Kiwango cha Ubora wa Majitaka ..... 9
2.6 Upotevu wa Maji ..... 10
2.7 Udhibiti wa Upotevu wa Maji ..... 11
2.8 Utendaji wa Kifedha ..... 12
2.9 Uwiano wa Watumishi na Wateja ..... 13
2.10 Huduma kwa Wateja ..... 14
2.11 Uwasilishaji wa Mipango na Taarifa ..... 14
2.12 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Taarifa iliyopita ..... 15
2.13 Utekelezaji wa Masharti ya Bei za Maji ..... 16
2.14 Utekelezaji wa Maagizo ya Ukaguzi ..... 16
2.15 Hali ya Menejimenti na Watumishi ..... 16

**SEHEMU YA TATU** ..... 17
**3.0 USHINDANISHAJI WA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI** ..... 17
3.1 Taratibu za ushindanishaji ..... 17
3.2 Matokeo ya Ushindanishaji ..... 17

**SEHEMU YA NNE** ..... 24
**4.0 MASUALA YALIYOBAINIKA NA MAPENDEKEZO** ..... 24

## NENO LA MWENYEKITI WA BODI

Upatikanaji wa huduma bora za majisafi, usafi wa mazingira pamoja na usimamizi thabiti wa huduma hizo hutengeneza fursa za uboreshaji wa mazingira na maendeleo kwa jamii. Aidha, huduma bora za majisafi, usafi wa mazingira na usimamizi thabiti wa rasilimali za maji husaidia ukuaji wa uchumi wa Taifa na hivyo kuchangia katika kutokomeza umaskini. Kwa msingi huu, ufuatiliaji wa utendaji wa kila mwaka wa Mamlaka za Maji ni muhimu sana.

Kwa kutambua umuhimu uliobainishwa, Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira (Mamlaka za Maji) kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Taarifa hii imeandaliwa kwa kuzingatia kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Sura Na 272.

Taarifa hii inakusudia kuwajulisha wadau wakiwemo wateja, Serikali, wafadhili na washirika wa maendeleo, takwimu sahihi na kwa uwazi utendaji wa mamlaka za maji kiufundi, kibiashara na kifedha kwa mwaka wa fedha 2022/23. Pamoja na kutambua maendeleo yaliyofikiwa na mamlaka za maji katika kutoa huduma, EWURA imedhamiria kuendeleza juhudi za kuhakikisha utendaji wa mamlaka za maji katika nchi yetu unazidi kuimarika.

Kukamilika kwa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 kumetokana na juhudi na ushirikiano wa taasisi mbalimbali na watu binafsi katika kuandaa na kukamilisha taarifa hii ya utendaji wa mamlaka za maji kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa msaada wake usio na kikomo kwa Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira nchini. Vile vile, napenda kutoa shukrani kwa Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) pamoja na Baraza la Ushauri la Watumuaji wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA-CCC). Mwisho, napenda kuipongeza Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wote wa EWURA waliofanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Prof. Mark J. Mwandosya
**Mwenyekiti wa Bodi**

Machi, 2024

## DIBAJI

Kwa miaka 15 mfululizo, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imekuwa ikiandaa taarifa za mwaka za utendaji wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira Tanzania bara. Madhumuni ya taarifa hizo ni kuujulisha umma kuhusu hatua iliyofikiwa na mamlaka za maji katika kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, kupima jitihada za mamlaka hizo katika kufikia malengo ya utendaji kazi na kupendekeza hatua za kuboresha utoaji wa huduma.

Taarifa hii inalinganisha utendaji wa mamlaka za maji 85 inayojumuisha mamlaka 25 za mikoa, miradi 7 ya kitaifa, mamlaka 47 za wilaya na mamlaka 6 za miji midogo. Aidha, taarifa imeshindanisha utendaji wa mamlaka za maji kwa kuzingatia utendaji wa jumla wa mamlaka za maji pamoja na juhudi za mamlaka za maji kufikia malengo waliojiwekea kwa mwaka wa fedha 2022/23. Ushindanishaji wa utendaji wa mamlaka za maji umegawanywa katika makundi matatu ambayo ni Kundi la I kwa mamlaka za maji zenye wateja zaidi ya 20,000, Kundi la II kwa mamlaka za maji zenye wateja kati ya 5,000 na 20,000, na Kundi la III kwa mamlaka za maji zenye wateja chini ya 5,000.

Kwa utendaji wa jumla (overall ranking), mamlaka za maji za Iringa, Nzega na Biharamulo ziliibuka kuwa mamlaka zilizofanya vizuri katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa Kundi la I, Kundi la II na Kundi la III, mtawalia.Alama za utendaji kwa mamlaka hizo ni asilimia 77.7, 83.3 na 75.4 kama Vizuri Sana kwa Iringa, Nzega na Biharamulo mtawalia. Kwa upande mwingine, mamlaka za maji za Rombo, Korogwe na Songe zimekuwa na utendaji usioridhisha katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa Kundi la I, Kundi la II na Kundi la III, mtawalia. Kwa upande wa ushindanishaji wa utendaji wa mamlaka za maji kwa kuzingatia kigezo cha juhudi za kufikia malengo yaliyomo kwenye mipango yao ya biashara (utility ranking), mamlaka za maji za Tabora, Lindi na Mbinga ziliibuka washindi kwa Kundi la I, Kundi la II na Kundi la III mtawalia.

Aidha, mamlaka za maji za Mwanza, Kahama na Bukoba zimekuwa na utendaji usioridhisha katika Kundi la I; Geita, Njombe na Korogwe kwa Kundi la II; na Mugango-Kiabakari, Chato, Chunya, Gairo, Ifakara, Kibaya, Kibondo, Kilindoni, Kilwa Masoko, Kiomboi, Kyela-Kasumulu, Liwale, Ludewa, Mahenge, Mwanhuzi, Namanyere, Namtumbo, Ruangwa, Rujewa, Songe, Tunduru, Ushirombo, Maganzo na Turiani kwa Kundi la III. EWURA inapongeza hatua iliyofikiwa na baadhi ya mamlaka za maji katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira. Hata hivyo, mamlaka za maji ambazo utendaji wao hauridhishi zinahimizwa kuongeza juhudi zaidi kufikia malengo yaliyowekwa na miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuhusu huduma za maji na usafi wa mazingira.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, utendaji wa mamlaka za maji kwa baadhi ya viashiria uliimarika. Uwezo wa miundombinu na uzalishaji wa maji uliimarika kwa asilimia 16.9 kutoka

mita za ujazo milioni 744 hadi mita za ujazo milioni 870, uzalishaji wa maji uliongezeka kwa asilimia 1.8 kutoka mita za ujazo milioni 393 hadi mita za ujazo milioni 400, wateja wa huduma ya maji waliongezeka kwa asilimia 11 kutoka wateja 1,385,485 hadi 1,532,362. Uwiano wa watumishi na wateja uliimarika kutoka 4.2 hadi 3.8 kwa kila wateja 1,000 na uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji iliongezeka kwa asilimia 8 kutoka asilimia 55 hadi hadi asilimia 63.

Hata hivyo, baadhi ya viashiria vya utendaji wa mamlaka za maji vilizorota, kama vile upotevu wa maji, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na uzingatiaji wa ubora wa majitaka. Taarifa pia inaonesha mapendekezo yanayolenga kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya utoaji huduma ya mamlaka za maji. EWURA inawashukuru wadau wote kwa kuiunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yake ya kiudhibiti. Vilevile, EWURA inatoa wito kuendelea kuimarishwa kwa ushirikiano katika kuhakikisha utendaji bora wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira nchini.

Dkt. James A. Mwainyekule
**Mkurugenzi Mkuu**

Machi, 2024

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BOD | Mahitaji ya Oksijeni Kibaiolojia (Biological Oxygen Demand) |
| COD | Mahitaji ya Oksijeni Kikemikali (Chemical Oxygen Demand) |
| DAWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam |
| *E. coli* | Kiashiria cha uchafuzi wa majisafi unaotokana na vimelea *(Escherichia coli)* |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| HTM | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni Trunk Main |
| IWA | Jumuiya ya Kimataifa ya Wataalam wa Maji *(International Water Association)* |
| KASHWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga |
| MajIS | Mfumo wa Uwasilishaji Taarifa za Maji Kielektroniki |
| Mamlaka ya Maji | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira |
| MANAWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea |
| RUWASA | Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini |

## VIPIMO NA ALAMA

| | |
|---|---|
| % | Asilimia |

## FASILI YA VIASHIRIA VIKUU VYA UTENDAJI

| NA. | KIASHIRIA | TAFSIRI | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| i. | Muda wa Ukusanyaji wa madeni | Wastani wa muda katika miezi ambayo wateja huchukua kulipa ankara. Inakokotolewa kwa kuchukua jumla ya madeni ambayo mamlaka ya maji inawadai wateja kutokana na huduma ya majisafi na majitaka kwa mwaka zikigawanywa na jumla ya mauzo ya maji na maji taka (ankara) ikizidishwa na miezi 12. Utendaji mzuri ni usiozidi miezi miwili (2) | Miezi |
| ii. | Wastani wa saa za huduma | Saa kwa siku ambazo mtumiaji anaweza kuchota maji kwenye bomba lililounganishwa moja kwa moja kwenye mtandao wa mamlaka ya maji. Kiwango bora cha huduma ni saa 24 | Saa |
| iii. | Matumizi ya umeme kwa kila mita ya ujazo ya maji inayozalishwa | Matumizi ya umeme katika mwaka kwa kugawanya na jumla ya mita za ujazo wa maji zinazozalishwa | kWh/mita za ujazo |
| iv. | Uwiano wa maunganisho ya maji yenye dira | Idadi ya maunganisho yenye dira za maji katika asilimia. Kiwango kinachotakiwa ni asilimia 100 | (%) |
| v. | Upotevu wa Maji | Tofauti kati ya kiasi cha maji kinachozalishwa na mamlaka ya maji au kinachonunuliwa kutoka mamlaka ya maji nyingine na kile kinachouzwa kwa watumiaji kama asilimia ya maji yanayozalishwa/nunuliwa. Inapendekezwa iwe chini ya asilimia 20 | (%) |
| vi. | Uwiano wa gharama za uendeshaji na uchakavu dhidi ya mapato | Uwiano kati ya gharama za uendeshaji na uchakavu wa miundombinu na mapato yanayozalishwa. Usimamizi mzuri wa fedha unahitaji uwiano uwe chini ya 0.8 | Uwiano |
| vii. | Uwiano wa gharama za watumishi kwa mapato ya mamlaka ya maji | Jumla ya gharama za watumishi kama asilimia ya makusanyo yote kutokana na ankara za majisafi na majitaka na shughuli zingine za uendeshaji katika mwaka husika. Gharama hizi hazijumuishi ruzuku | Asilimia |
| viii. | Uwiano wa idadi ya watu waliopo kwenye eneo lenye mtandao wa maji | Uwiano unapatikana kwa kugawa idadi ya watu waliopo ndani ya mita 200 kutoka kwenye bomba la usambazaji wa maji kwa idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma | Asilimia |

| NA. | KIASHIRIA | TAFSIRI | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| ix. | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji | Uwiano unapatikana kwa kugawa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji kwenye maunganisho ya majumbani, kwenye magati/vilula na kwenye taasisi za bweni dhidi ya idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma.<br><br>Idadi ya watu wanaohudumiwa majumbani na kwenye magati/vilula hupatikana kwa kuzidisha idadi ya maunganisho ya majumbani na kwenye magati/vilula kwa wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma kwenye maunganisho hayo. Aidha, idadi ya watu wanaohudumiwa na taasisi za bweni hupatikana kwa kujumlisha watu wote wanaoishi kwenye taasisi hizo | Asilimia |
| x. | Ufanisi wa ukusanyaji mapato | Uwiano wa jumla ya makusanyo kwa jumla ya ankara katika asilimia hukokotolewa kwa kugawanya kiasi cha mapato yaliyokusanywa kwa kiasi cha ankara kilichotozwa kikizidishwa na 100 | Asilimia |
| xi. | Tija ya watumishi | Idadi ya watumishi kwa kila maunganisho 1,000 ya majisafi na majitaka. Inakokotolewa kwa kugawa jumla ya watumishi kwa jumla ya maunganisho ya majisafi na majitaka ikizidishwa na 1,000. Kiwango kinachofaa ni chini ya watumishi watano kwa kila maunganisho 1,000 | Idadi ya watumishi kwa kila maunganisho 1,000 |
| xii. | Kukidhi viwango vya ubora wa maji | Uwiano wa sampuli za maji zilizopimwa na kukidhi viwango vya ubora. Hupatikana kwa kugawanya idadi ya sampuli zilizokidhi viwango kwa idadi ya sampuli zilizopimwa na kuzidisha kwa 100. Kiwango kinachofaa ni angalau 98% | Asilimia |
| xiii. | Uwiano wa uendeshaji | Uwiano kati ya gharama za uendeshaji na mapato yanayozalishwa. Usimamizi mzuri wa fedha unahitaji uwiano uwe chini ya 0.67 | Uwiano |
| xiv. | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya majitaka | Uwiano unapatikana kwa kugawa idadi ya watu wanaopata huduma ya majitaka kwenye maunganisho ya majumbani na kwenye taasisi za bweni dhidi ya idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma.<br><br>Idadi ya watu wanaohudumiwa majumbani hupatikana kwa kuzidisha idadi ya maunganisho ya majumbani kwa wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma kwenye maunganisho hayo. Aidha, idadi ya watu wanaohudumiwa kwenye taasisi za bweni hupatikana kwa kujumlisha watu wote wanaoishi kwenye taasisi hizo | Asilimia |
| xv.. | Kukidhi viwango vya ubora wa majitaka | Uwiano wa sampuli za majitaka zilizopimwa na kukidhi viwango vya ubora. Hupatikana kwa kugawanya idadi ya sampuli zilizopimwa na kukidhi viwango kwa idadi ya sampuli zilizopimwa na kuzidisha kwa 100. Kiwango kinachofaa ni angalau 95% | Asilimia |

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Sehemu hii inatoa taarifa ya utangulizi kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Majukumu yake katika kusimamia Sekta ya Maji, Dira na Dhamira ya EWURA, Lengo la Taarifa, Maelezo kuhusu Mamlaka za Maji na Mbinu za uandaaji wa Taarifa.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) iliundwa mwaka 2001 kwa mujibu wa Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na kuanza kazi Septemba 2006. Kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Sheria hiyo, majukumu ya Mamlaka ni pamoja na:

a) kutekeleza kazi zote zilizoainishwa kwenye Sheria ya EWURA na Sheria za Kisekta;
b) kutoa, kuhuisha na kufuta leseni;
c) kuweka na kusimamia viwango vya ubora wa huduma;
d) kudurusu na kusimamia bei za huduma;
e) kutunga sheria ndogo na kanuni;
f) kufuatilia maendeleo ya sekta zinazodhibitiwa kwa kuzingatia upatikanaji, ubora wa huduma, gharama ya huduma, ufanisi wa uzalishaji, uwekezaji na usambazaji wa huduma;
g) kusimamia utatuzi wa malalamiko na migogoro;
h) kutoa taarifa kuhusu kazi za udhibiti;
i) kupata maoni ya mamlaka zingine za kiudhibiti; na
j) kusimamia utekelezaji wa Sura Na 414 iliyoanzisha EWURA.

## 1.1 Majukumu ya EWURA katika Sekta ya Maji

Katika kusimamia Sekta ya Maji, EWURA inaongozwa na Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 *[Sheria ya Maji (2019)]*. Kwa mujibu wa Kifungu cha 28 cha Sheria hiyo, EWURA imepewa mamlaka ya kudhibiti huduma zinazotolewa na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira nchini. Majukumu hayo ni pamoja na:

a) Utoaji wa leseni kwa watoa huduma za maji na usafi wa mazingira na kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni hizo;
b) kutoa miongozo na kanuni mbalimbali kuhusu utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira;
c) kuchambua na kuidhinisha bei za huduma za maji na usafi wa mazingira;
d) kufuatilia ubora wa maji;
e) kukusanya na kuchambua taarifa za utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira;
f) kufanya stadi mbalimbali kwa ajili ya masuala ya kiutawala na kiuendeshaji katika sekta ya maji; na
g) kuandaa ripoti ya mwaka ya utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira.

Katika kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Sekta ya Maji, EWURA imeandaa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ikiwa ni taarifa ya 15 katika mfululizo wa taarifa za utendaji wa mamlaka za maji zilizoandaliwa. Taarifa hii inalinganisha utendaji wa mamlaka za maji 85 inayojumuisha mamlaka 25 za mikoa, miradi ya kitaifa 7, mamlaka za wilaya 47 na mamlaka 6 za miji midogo. Utayarishaji wa taarifa hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sura Na. 272 kinachoitaka EWURA kuandaa taarifa ya uchambuzi linganishi wa utendaji wa mamlaka za maji kila mwaka.

## 1.2 Dira ya EWURA

***"Kuwa Mdhibiti wa Kiwango cha Kimataifa kwa Huduma Endelevu za Nishati na Maji".***

## 1.3 Dhamira ya EWURA

***"Kudhibiti huduma za nishati na maji kwa uwazi, ufanisi na tija ili kuhakikisha ubora, upatikanaji na unafuu wa huduma hizo".***

## 1.4 Lengo la Taarifa

Lengo kuu la taarifa hii ni kuonesha utendaji wa jumla wa mamlaka za maji kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa kuzingatia takwimu muhimu za utendaji na viashiria katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira. Taarifa pia inaonesha masuala muhimu yaliyobainika na mapendekezo yanayolenga kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya utoaji huduma ya mamlaka za maji.

Kwa kuzingatia Mwongozo wa Vigezo vya Utendaji wa EWURA kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2022, tathmini ilifanyika kwa kuangalia utendaji wa jumla (overall ranking) katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira wa mamlaka za maji na utendaji kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya mamlaka hizo katika mipango yao ya biashara (utility ranking).

Ushindanishaji wa utendaji wa mamlaka za maji umegawanywa katika makundi matatu. Kundi la I ni mamlaka za maji zenye wateja zaidi ya 20,000, Kundi la II ni mamlaka za maji zenye wateja kati ya 5,000 na 20,000, na Kundi la III ni mamlaka za maji zenye wateja chini ya 5,000.

Taarifa na takwimu zilizotumika zilipatikana kutoka mamlaka za maji kupitia taarifa zao za mwaka za utendaji, taarifa za utendaji kupitia mfumo wa kielektroniki (MajIS), ukaguzi na ufuatiliaji wa utendaji kazi, mipango ya biashara na mikutano ya mashauriano na Wizara ya Maji, Wizara ya Afya na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Michango mingine kwenye taarifa ilitokana na ufafanuzi uliotolewa na mamlaka za maji

kuhusu mwenendo na matokeo ya utendaji wao wakati wa ukaguzi wa ufanisi uliofanywa na EWURA. Pia Baraza la Ushauri wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA-CCC) lilishirikishwa katika kutoa maoni ya taarifa hii kabla ya kuchapishwa. Maelezo kuhusu mamlaka za maji na mbinu za uandaaji taarifa hii vimewasilishwa katika sehemu 1.5 na 1.6 ya taarifa hii.

Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni (i) Utangulizi (ii) Uchambuzi wa Utendaji wa Mamlaka za Maji (iii) Ushindanishaji wa Utendaji na (iv) Masuala muhimu yaliyobainika na Mapendekezo.

## 1.5 Maelezo kuhusu Mamlaka za Maji

Mamlaka za maji zinafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Sura Na. 272 na kudhibitiwa na EWURA kwa mujibu wa sheria hiyo. Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira, mamlaka za maji zinatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia leseni zinazotolewa na EWURA. Leseni hizo zipo katika madaraja matatu ambayo ni Daraja la I, Daraja la II na Daraja la III. Mamlaka za maji ambazo hazikidhi vigezo vya kupata madaraja hayo ya leseni hupatiwa leseni za muda.

Katika mwaka wa mapitio, mamlaka za maji za Tanga na Moshi zimeendelea kutoa huduma kwa kutumia leseni za Daraja la I, wakati mamlaka za maji za Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya na Iringa zikiendelea kushikilia Leseni za Daraja la II na mamlaka za maji za Babati, KASHWASA na Kahama zikipandishwa hadhi na kuwa na Leseni Daraja la II.

Kwa ujumla, mamlaka za maji 64 zilikuwa zikifanya kazi chini ya Leseni za Daraja la III, huku mamlaka za maji 11, ambazo ni Busega, Kyela-Kasumulu, Kibondo, Itumba-Isongole, Tukuyu, Chunya, Namanyere, Namtumbo, Rujewa, Tunduma, na Rombo zikifanya kazi chini ya Leseni ya Muda.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 5 (1) ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019, mamlaka za maji zimepangwa katika madaraja manne, ambayo ni AA, A, B na C kulingana na uwezo wao wa kifedha na utoaji wa huduma za majisafi. Mamlaka za maji zilizojadiliwa katika taarifa hii na madaraja yake, madaraja ya leseni ya usambazaji majisafi na usafi wa mazingira na maeneo yao ya huduma yameoneshwa kwenye Jedwali Na. 1.

## Jedwali Na. 1: Mgawanyo wa Mamlaka za Maji kwa kuzingatia Leseni, Madaraja na Kundi la Mamlaka

| Madaraja ya Leseni | | Madaraja ya Mamlaka | | Kundi la Mamlaka | |
|---|---|---|---|---|---|
| Daraja la Leseni | Idadi ya Mamlaka | Daraja | Idadi ya Mamlaka | Kundi | Idadi ya Mamlaka |
| I | 2 | AA | - | Kundi la I (wateja zaidi ya 20,000) | 19 |
| II | 8 | A | 19 | Kundi la II (wateja kati ya 5,000 - 20,000 | 18 |
| III | 64 | B | 5 | Kundi la III (wateja chini ya 5,000) | 48 |
| Ya Muda | 11 | C | 60 | | |

*DAWASA haikuwa na Daraja

## Fasili ya Madaraja ya Leseni

| | |
|---|---|
| **Daraja la I** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma mwenye uwezo wa kiufundi, kiuendeshaji na mwenye uwezo wa kurejesha gharama zote za uendeshaji |
| **Daraja la II** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma mwenye uwezo wa kiufundi, kiuendeshaji na mwenye uwezo wa kurejesha gharama za uendeshaji isipokuwa sehemu ya gharama za uwekezaji |
| **Daraja la III** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma ambaye bado anasaidiwa na Serikali kifedha, kiuendeshaji na kiufundi na ana uwezo wa kurejesha kiasi cha gharama zake za uendeshaji |
| **Leseni ya Muda** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma ambaye hajakidhi vigezo vya kupata leseni ya Daraja la I, II au III (mwenye miundombinu na rasilimali watu kwa ajili ya utoaji wa huduma) |

## Fasili ya Madaraja ya Mamlaka za Maji

| | |
|---|---|
| **AA** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wake na zinamudu gharama za uendeshaji, matengenezo, uchakavu, na zinaweza kurudisha gharama za uwekezaji |
| **A** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 75 ya wakazi wake na zinamudu gharama zote za uendeshaji, matengenezo na uchakavu |
| **B** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 65 na zinamudu gharama zote za uendeshaji na matengenezo |
| **C** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji chini ya asilimia 65 na zinamudu gharama za uendeshaji na matengenezo isipokuwa sehemu ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo inagharamiwa na Serikali |

## 1.6 Mbinu za Uandaaji wa Taarifa

Maandalizi ya taarifa hii yalihusisha ukusanyaji,uchambuzi na uhakiki wa taarifa za kiufundi, kibiashara na kifedha kutoka mamlaka za maji. Takwimu na taarifa pia zilipatikana kutoka kwenye taarifa za kila mwezi za utendaji kupitia mfumo wa kielektroniki (MajIS), taarifa za utendaji za mwaka, taarifa za fedha na mipango ya biashara. Taarifa na takwimu zilizotumika zilihakikiwa kupitia mchakato ufuatao:

a) Kufanya ukaguzi kwenye mamlaka za maji;
b) Ufafanuzi kutoka kwa mamlaka za maji pale ambapo takwimu zilionesha matokeo yasiyo ya kawaida ikilinganishwa na taarifa za awali au ambapo takwimu au maelezo yalikuwa na mashaka;
c) Kufanya mikutano ya mashauriano na watendaji wakuu wa mamlaka za maji ili kujadili na kuthibitisha taarifa na takwimu zilizopokelewa kabla ya kuchapishwa. Aidha, mikutano hiyo ilijumuisha pia Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, na RUWASA;
d) Kufanya mikutano ya mashauriano na Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, na RUWASA ili kujadili rasimu ya taarifa;
e) Mashauriano na Pia Baraza la Ushauri wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA-CCC).


# SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTENDAJI

Sehemu hii inatoa uchambuzi wa masuala ya kiufundi; kibiashara na kiusimamizi ya mamlaka za maji kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa kulinganisha utendaji uliofikiwa katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/21.

## 2.1 Uzalishaji na Mahitaji ya Maji

Kwa miaka mitatu iliyopita, mahitaji ya jumla ya maji, uwezo wa miundombinu na uzalishaji wa maji umekuwa ukiendelea kuongezeka.





Katika mwaka wa fedha 2022/23, mahitaji ya maji, uwezo wa miundombinu na uzalishaji wa maji uliongezeka kwa asilimia 4, 16.94 na 1.78 mtawalia ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/22. Licha ya kuongezeka kwa uzalishaji wa maji katika mwaka wa fedha 2022/23, uzalishaji wa maji kwa jumla ulikuwa asilimia 49 tu ya mahitaji yote ya maji ndani ya maeneo ya mamlaka za maji. Ongezeko la mahitaji ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka za maji linahusishwa zaidi na ongezeko la watu kufuatia upanuzi wa maeneo ya huduma za mamlaka za maji na ongezeko la kawaida la idadi ya watu.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, uwiano wa uzalishaji wa maji na uwezo wa mitambo ya uzalishaji wa maji unaonesha kuzorota. Uwiano ulishuka hadi asilimia 46 katika mwaka wa fedha 2022/23 kutoka asilimia 63 katika mwaka wa fedha 2020/21. Matumizi ya chini ya uwezo wa mitambo hiyo ulitokana na mtandao mdogo wa usambazaji maji, na kukatika kwa umeme mara kwa mara katika vituo vya uzalishaji maji.

## 2.2 Kiwango cha Upatikanaji wa Maji

### a. Upatikanaji wa huduma ya maji

Kwa mwaka wa fedha 2022/23, uwiano wa idadi ya watu waliopo kwenye eneo lenye mtandao wa maji ulikuwa asilimia 82 ikilinganishwa na asilimia 83 katika mwaka wa fedha 2021/22 na asilimia 82 katika mwaka wa fedha 2020/21. Kwa upande mwingine, uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji uliongezeka hadi asilimia 63 ikilinganishwa na asilimia 55 katika mwaka wa fedha 2021/22 na asilimia 56 katika mwaka wa fedha 2020/21.





Uchambuzi wa idadi ya watu wanaoishi katika eneo lenye mtandao wa maji unaonesha kuwa:

i. Mamlaka za maji za DAWASA, Iringa, Tabora, Tanga, Kigoma, Sumbawanga, Njombe, Wanging'ombe, Igunga, Nzega, Sengerema, na Makambako zilifikia asilimia 90 ya huduma ya mtandao wa maji; na

ii. Mamlaka za maji za Kibaya, Maganzo, Mafinga, Gairo, Songe, Ngara, Ifakara, Lindi, Maswa, Same-Mwanga, Mwanza, na Utete zilikuwa na upungufu wa zaidi ya asilimia 10 wa uwiano wa idadi ya watu wanaoishi katika eneo lenye mtandao wa maji kutokana na upanuzi wa maeneo ya huduma.


### b. Muda wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji




Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, wastani wa muda wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa siku umeendelea kubaki saa 14. Wastani huo ni chini ya kiwango kinachotakiwa cha saa 24. Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, mamlaka za maji za KASHWASA, Songea, Kahama, Nzega, Igunga, Orkesumet na Turiani zilikuwa na usambazaji wa maji kwa wastani wa saa 24 zinazotakiwa. Aidha, mamlaka za maji za KASHWASA, Songea, Kahama, Nzega, Igunga na Turiani ziliendelea na usambazaji wa maji kwa wastani wa saa 24 kwa miaka mitatu mfululizo. Hata hivyo, mamlaka za maji nne ambazo ni HTM, Kibaya, Korogwe na Songe zilikuwa na usambazaji wa maji chini ya saa tano kwa siku. Uchambuzi unaonyesha kuwa, kupungua kwa saa za huduma miongoni mwa mamlaka za maji kulichangiwa zaidi na kupungua kwa uzalishaji wa maji na kukatika kwa umeme mara kwa mara.

## 2.3 Kiwango cha Ubora wa Maji

### a. Miundombinu ya Kusafisha na Kutibu Maji





Katika mwaka wa fedha 2022/23, asilimia 94 ya mamlaka za maji zilikuwa na miundombinu

ya kutibu maji ikilinganishwa na asilimia 91 na 88 katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/21 mtawalia. Ili kuhakikisha majisafi na salama yanawafikia wateja, katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 80 zilitibu maji kwa kutumia mitambo pamoja na dawa mbalimbali za kuua vimelea vya wadudu kwenye maji kama vile *calcium hypochlorite*. Vilevile, mamlaka za maji za Mombo, Namanyere, Songe, Tunduma na Tunduru hazikuwa na miundombinu ya kutibu maji, ikilinganishwa na mamlaka za maji nane na 11 katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/21 mtawalia.

### b. Ubora wa Maji

Katika mwaka wa fedha 2022/23, kiwango cha ubora wa maji yanayosambazwa na mamlaka za maji kwa kuzingatia vimelea vya wadudu (*E. coli)* na kiwango cha tope (*turbidity*) viliimarika na kufikia asilimia 84 na asilimia 86 mtawalia.





Kiwango cha asidi (pH) kilishuka kufikia asilimia 92 ikilinganishwa na asilimia 94 ya mwaka 2021/22. Aidha, kiwango cha dawa (*residual chlorine*) kilishuka kufikia asilimia 24 ikilinganishwa na asilimia 30 kwa mwaka 2021/22 na asilimia 34 kwa mwaka 2020/21.

## 2.4 Upatikanaji wa Huduma za Usafi wa Mazingira

### a. Huduma za Majitaka kwa Njia ya Mtandao

Katika mwaka wa fedha 2022/23, idadi ya wateja wanaopata huduma ya majitaka kupitia mtandao wa bomba ilifikia 56,899 kutoka 55,996 katika mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, uwiano wa watu wanaopata huduma ya majitaka kwa njia ya mtandao wa bomba kutoka katika mamlaka za maji 11 zinazotoa huduma hiyo ambazo ni Arusha, DAWASA, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Songea, Tabora na Tanga umefikia asilimia 10.7 ya idadi ya watu katika maeneo ya huduma ya mamlaka hizo.




Uwiano huo umeshuka kutoka asilimia 13.1 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Sababu ya kushuka kwa uwiano huo ni kutokana na baadhi ya mamlaka za maji kuongeza eneo la kutoa huduma.

### b. Huduma ya Majitaka Nje ya Mtandao

Katika mwaka wa fedha 2022/23, asilimia 97.72 ya kaya zilizo ndani ya maeneo ya huduma ya mamlaka za maji zilikuwa na vyoo na asilimia 1.32 hazikuwa na vyoo. Aidha, asilimia 0.96 ya kaya zilipata huduma ya majitaka kwa njia ya mtandao wa majitaka kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya 2.4(a) ya taarifa hii.

## 2.5 Kiwango cha Ubora wa Majitaka

### a. Miundombinu ya Kutibu Majitaka na Topekinyesi

Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 21 zilikuwa na miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi ikilinganishwa na mamlaka za maji 18 katika mwaka wa fedha 2021/22. Mamlaka hizo ni Arusha, Dodoma, Moshi, Morogoro, Mwanza, Iringa, Songea, Mbeya, Tabora, DAWASA, Sumbawanga, Bukoba, Geita, Kigoma, Musoma, Kahama, Shinyanga, Lindi, Nzega, Sengerema na Busega.


Aidha, mamlaka za maji tisa, ambazo ni Tabora, Tanga, Singida, Babati, Njombe, Bunda, Chato, Igunga na Korogwe ziliendelea na ujenzi wa miundombinu wakati mamlaka za maji 10, ambazo ni DAWASA, Gairo, Mbinga, Namanyere, Ludewa, Itumba-Isongole, Kondoa, Mafinga, Mpwapwa na Utete zilikuwa na maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo. DAWASA inatarajia kuanza ujenzi wa miundombinu ya ziada ya kutibu majitaka kufuatia kuongezeka kwa huduma.

Hata hivyo, jumla ya mamlaka za maji 45 hazikuwa na miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi wala maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo. Mamlaka hizo ni Bariadi, Mpanda, Vwawa-Mlowo, HTM, KASHWASA, Makonde, MANAWASA, Maswa, Mugango-Kiabakari, Wanging'ombe, Biharamulo, Chunya, Ifakara, Karatu, Kasulu, Kibaya, Kibondo, Kilindoni, Kilwa Masoko, Kiomboi, Kishapu, Kyela-Kasumulu, Liwale, Loliondo, Lushoto, Mahenge, Makete, Manyoni, Mbulu, Mwanhuzi, Namtumbo, Ngara, Orkesumet, Ruangwa, Rujewa, Same-Mwanga, Songe, Tukuyu, Tunduru, Ushirombo, Maganzo, Makambako, Mombo, Turiani, na Rombo.

### b. Ubora wa Majitaka

Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 21 ambazo ni Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Songea, Kahama, Shinyanga, Arusha, Iringa, DAWASA, Tabora, Sengerema, Nzega, Bukoba, Lindi, Kigoma, Busega, Dodoma, Geita, Sumbawanga na Musoma zilikua

na miundombinu ya kutibu majitaka. Kati ya mamlaka hizo, 12 ambazo ni Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Songea, Kahama, Shinyanga, Arusha, Iringa, DAWASA, Dodoma na Geita ziliweza kupima ubora wa majitaka yaliyotibiwa na kurudishwa kwenye mazingira (*effluent*).





Vilevile, Mamlaka za maji 7, ambazo ni Tabora, Sengerema, Nzega, Bukoba, Lindi, Kigoma, na Busega hazikuweza kupima ubora wa majitaka kutokana na kiwango kidogo cha majitaka waliyopokea hivyo kutokua na majitaka yaliyotiririshwa kwenye mazingira (*effluent*). Hata hivyo, mamlaka za maji za Musoma na Sumbawanga hazikupima ubora wa majitaka licha ya kutakiwa kufanya hivyo.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kumekuwa na kupanda na kuimarika kwa kiwango cha ubora wa majitaka yaliyotibiwa na kurudishwa kwenye mazingira (*effluent*). Viwango hivyo vimeangaliwa kwa kuzingatia viashiria vya mahitaji ya oksijeni kibaiolojia (BOD) na kikemikali (COD).

Katika mwaka wa fedha 2022/23, hali ya kukidhi mahitaji ya oksijeni kibaiolojia iliongezeka hadi kufikia asilimia 58 ikilinganishwa na asilimia 46 kwa mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/2021 mtawalia. Aidha, hali ya kukidhi mahitaji ya oksijeni kikemikali iliongezeka hadi asilimia 50 ikilinganishwa na asilimia 46 na 41 iliyofikiwa katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/21 mtawalia.

## 2.6 Upotevu wa Maji

Kiwango cha upotevu wa maji kimeongezeka kwa asilimia 1.7 katika mwaka wa fedha 2022/23 ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 2.3 katika mwaka wa fedha 2021/22. Kiwango kikubwa cha upotevu wa maji kilichangiwa na mamlaka za maji kuwa na utekelezaji hafifu wa mikakati ya kupunguza upotevu wa maji. Katika mwaka wa mapitio, mamlaka za maji 10, ambazo ni Kishapu, Maganzo, Busega, Nzega, KASHWASA, Mwanhuzi, Kasulu, Rujewa, Igunga na Kahama zilikuwa na upotevu wa maji chini ya asilimia 20.



Wakati mamlaka za maji 13, ambazo ni Mahenge, Arusha, Mpanda, Vwawa-Mlowo, Makonde, Mpwapwa, Itumba-Isongole, Ifakara, Kiomboi, Rombo, HTM, Ushirombo na Mugango-Kiabakari zilikuwa na upotevu wa maji wa zaidi ya asilimia 50.

## 2.7 Udhibiti wa Upotevu wa Maji

Kwa mujibu wa Mwongozo wa EWURA wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021, mamlaka za maji zinatakiwa kuhakikisha upotevu wa maji hauzidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa. Aidha, kwa mujibu wa Mwongozo wa Kuchagua, Kufunga, Kupima pamoja na Kufanyia Matengenzo Dira za Maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021, mamlaka za maji zinatakiwa kuwa na sera ya dira za maji na kanzidata. Lengo la miongozo hii yote ni kudhibiti upotevu wa maji. Katika kufikia azma hii, uchambuzi umefanyika katika viashiria vifuatavyo:

### a. Mkakati wa kupunguza Upotevu wa Maji

Mwongozo wa EWURA wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021 unazitaka mamlaka za maji kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa maji. Mwongozo pia unasisitiza juu ya kuandaa mizania ya kupima viwango vya upotevu wa maji kwa mujibu wa mwongozo wa Jumuiya ya Kimataifa ya MajI (IWA) ili kujua maeneo ya upotevu wa maji kwenye mamlaka hizo za maji. Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 17 kati ya 85, ambazo ni DAWASA, Kahama, Moshi, Musoma, Shinyanga, Tanga, Bukoba, Bariadi, Makonde, Maswa, Biharamulo, Bunda, Igunga, Ngara, Nzega, Utete na Busega zilikuwa na Mkakati wa Kupunguza Upotevu wa Maji na mamlaka za maji zote 85 ziliandaa mizania ya kupima viwango vya upotevu wa maji.

### b. Sera ya Dira za Maji

Sera ya dira ya maji inalenga kuweka mfumo wa usimamizi wa dira za maji katika maeneo ya huduma ya mamlaka za maji. Pamoja na mambo mengine, sera inalenga kuweka mfumo maalum wa ufungaji wa dira za maji za wateja na hivyo kusaidia katika kudhibiti wa upotevu wa maji. Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 18 kati ya 85, ambazo ni DAWASA, Iringa, Kahama, Musoma, Mwanza, Shinyanga, Bukoba, Bariadi, KASHWASA, Makonde, Maswa, Biharamulo, Bunda, Igunga, Ngara, Nzega, Utete na Busega zilikuwa na sera ya dira za maji zilizoidhinishwa kwa ajili ya usimamizi wa dira za maji.

### c. Kanzidata ya Dira za Maji

Kanzidata ya dira za maji ni nyenzo muhimu katika kudhibiti upotevu wa maji. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Kuchagua, Kufunga, Kupima pamoja na kufanyia matengenezo dira za maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021, Mamlaka za maji zinapaswa kuwa na kanzidata ya

dira za maji. Lengo la kuwa na kanzidata ni kuwezesha mamlaka za maji kufahamu maeneo ambayo dira za maji zimefungwa na hivyo kurahisisha katika usomaji wa dira hizo pamoja na kudhibiti uvujaji pale inaporipotiwa. Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 6 kati ya 85, ambazo ni Musoma, Mwanza, Wanging'ombe, Biharamulo, Chunya na Makonde zilikuwa na kanzidata ya dira za maji.


### d. Uwiano wa Maunganisho yaliyofungwa Dira za Maji

Katika mwaka wa mapitio, uwiano wa maunganisho yaliyofungwa dira za maji uliimarika na kufikia asilimia 92 ikilinganishwa na asilimia 90 katika mwaka wa fedha 2021/22 na asilimia 87 katika mwaka wa fedha 2020/21. Uwiano huu bado uko chini ya kiwango cha huduma kinachokubalika cha asilimia 100. Katika Mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 62 kati ya 85 zilifikia asilimia 100 ya ufungaji wa dira za maji kwa wateja wake, wakati Mamlaka ya Maji ya Kyela-Kasumulu ilikuwa na uwiano wa chini wa asilimia 1. Vilevile, mamlaka za maji za Ludewa, Mombo, Tunduma na Namtumbo zilikua na ongezeko la juu kwa zaidi ya asilimia 10 la uwiano wa maunganisho yaliyofungwa dira za maji.

## 2.8 Utendaji wa Kifedha

### a. Ukusanyaji wa Mapato


Katika mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya mapato yaliyokusanywa kutokana na huduma ya majisafi na majitaka na shughuli nyingine za mamlaka za maji yameshuka kwa asilimia mbili ikilinganishwa na ongezeko la asilimia saba katika mwaka wa fedha 2021/22.




### b. Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato


Ufanisi katika ukusanyaji wa mapato kwa mamlaka za maji umesalia kuwa wastani wa asilimia 91 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021/22.

Aidha, Mamlaka ya Maji ya Vwawa-Mlowo ilikuwa na ufanisi wa chini zaidi wa ukusanyaji mapato wa chini ya asilimia 30.




### c. Wastani wa Bei za Maji

Wastani wa bei za maji uliongezeka kutoka Shilingi 1,276 kwa mita ya ujazo katika mwaka wa fedha 2021/22 hadi Shilingi 1,382 katika mwaka wa fedha 2022/23. Pamoja na wastani huo, bei za maji katika mwaka wa fedha 2022/23 zilitofautiana kati ya mamlaka za maji na zilikuwa kati ya Shilingi 300 hadi Shilingi 3,590 kwa mita ya ujazo. Utofauti wa bei umetokana na baadhi ya mamlaka za maji kutumia bei zilizopitishwa mwaka 2011 ambazo haziendani na gharama za uendeshaji kwa sasa.





### d. Uwiano wa Mapato na Gharama za Uendeshaji

Katika mwaka wa fedha 2022/23, wastani wa uwiano wa uendeshaji (working ratio) wa mamlaka za maji ulizorota hadi uwiano wa 1.3 kutoka uwiano wa 1.1 wa mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, uwiano wa gharama za uendeshaji na uchakavu dhidi ya mapato (operating ratio) ulizorota na kufikia 2.0 ikilinganishwa na 1.6 katika mwaka wa fedha 2021/22. Kuongezeka kwa uwiano huu kunamaanisha mamlaka za maji nyingi zimepunguza uwezo wa kujiendesha kutokana na mapato yake.




## 2.9 Uwiano wa Watumishi na Wateja

Katika kipindi cha mapitio, uwiano wa tija ya watumishi kwa kuzingatia idadi ya watumishi kwa kila maunganisho 1,000 ya majisafi na majitaka umeimarika. Uwiano uliimarika hadi 3.8 katika mwaka wa fedha 2022/23 ikilinganishwa na 4.2 na 4.5 katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/21, mtawalia. Mamlaka za maji zimeendelea kufanya vizuri katika kiashiria hiki cha utendaji kwa kuwa na kiwango kinachokubalika cha chini ya watumishi 5 kwa kila maunganisho 1,000.



## 2.10 Huduma kwa Wateja

Kanuni Na. 59 (1) ya Kanuni za Huduma ya Maji, inazitaka Mamlaka za Maji kuandaa na kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Katika mwaka wa mapitio, jumla ya mamlaka za maji 82 zilikuwa na Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Mamlaka ambazo hazikuwa na mkataba huo ni Kilwa Masoko, Liwale na Ruangwa. Katika taarifa hii, tathmini ya utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja imefanyika kwa kuzingatia mambo makuu mawili ambayo ni; uwepo wa mfumo mahususi wa kusajili malalamiko pamoja na kiwango cha utatuzi wa malalamiko ya wateja katika mamlaka za maji. Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji zote 85 zilikuwa na mifumo mahususi ya kusajili na kushughulikia malalamiko ya wateja. Mifumo hiyo huwezesha kupokea, kushughulikia na kutoa mrejesho wa malalamiko yanayosajiliwa. Aidha, tathmini ya kiwango cha ufuatiliaji wa malalamiko kinaonesha kuwa, jumla ya malalamiko 373,800 yalisajiliwa na mamlaka za maji katika mwaka wa fedha 2022/23. Malalamiko mengi yaliyosajiliwa yalihusu ukosefu wa maji, msukumo mdogo na mivujo ya maji. Kati ya malalamiko yaliyosajiliwa, malalamiko 356,498, sawa na asilimia 95.4 yalitatuliwa.

## 2.11 Uwasilishaji wa Mipango na Taarifa

### a. Uwasilishaji wa Mipango ya Biashara na Programu za Ufuatiliaji wa Ubora wa Majisafi na Majitaka

Katika mwaka wa mapitio, mamlaka za maji 57 kati ya 85 zilikuwa na mipango hai ya biashara (*approved business plans*). Mamlaka za maji ambazo hazikuwa na mpango wa biashara ni Mwanza, Bukoba, Geita, Njombe, Mugango-Kiabakari, Chato, Chunya, Gairo, Ifakara, Kibaya, Kibondo, Kilindoni, Kilwa-Masoko, Kiomboi, Korogwe, Kyela-Kasumulu, Liwale, Ludewa, Mahenge, Namanyere, Namtumbo, Ruangwa, Songe, Tunduru, Ushirimbo, Maganzo, Turiani na Kahama. Vilevile, Mamlaka za maji 78 kati ya 85 zilikuwa na programu za ufuatiliaji wa ubora wa majisafi na majitaka wakati mamlaka za maji za MANAWASA, Kilindoni, Kilwa-Masoko, Liwale, Mahenge, Utete na Turaini hazikuwa na programu hiyo.

### b. Uwasilishaji wa Taarifa

Kwa miaka mitatu mfululizo, mamlaka za maji za Mwanza, Songea na Rujewa zimewasilisha taarifa zote kwa wakati. Tathmini ya uwasilishaji wa taarifa ilifanyika kwa kuzingatia uwasilishaji wa taarifa za mwaka na mwezi kwa njia ya kielektroniki (MajIS), pamoja na taarifa za kiufundi na kifedha kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

### Jedwali Na. 2 Hali ya Uwasilishaji wa Taarifa

| Maelezo | Idadi ya Taarifa zinazotakiwa | Idadi ya Taarifa zilizowasilishwa kwa wakati | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
| Taarifa za Kila Mwezi za MajIS | 1,020 | 532 | 628 | 752 |
| Taarifa za Mwaka za MajIS | 85 | 54 | 54 | 53 |
| Taarifa za Kiufundi | 85 | 62 | 64 | 54 |
| Taarifa za Fedha | 85 | 64 | 72 | 63 |

## 2.12 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Taarifa iliyopita

Katika taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, jumla ya mapendekezo nane yafuatayo yalitolewa:

a) Mamlaka za maji kuweka na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha kiwango cha dawa katika maji kinakidhi viwango vya ubora;
b) Mamlaka za maji za wilaya na miji midogo ziajiri watumishi wenye sifa stahiki za kusimamia ubora wa maji na kuhakikisha kuwa watumishi wenye weledi na ujuzi wanahusika katika mchakato wa uwekaji dawa kwenye maji;
c) Mamlaka za maji za mikoa na miradi ya kitaifa zichukue hatua na kuhakikisha uboreshaji katika viashiria vya viwango vya mahitaji ya oksijeni kibiolojia na kikemikali (BOD na COD) kwenye majitaka yaliyotibiwa na kurudishwa kwenye mazingira (effluent);
d) Mamlaka za maji kuchukua hatua za kuhakikisha upotevu wa maji hauzidi kiwango kinachokubalika cha chini ya asilimia 20. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa maji kwa mujibu wa Mwongozo wa EWURA wa Kuandaa Mkakati wa Kupunguza Upotevu wa Maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021;
e) Mamlaka za maji kubuni na kutekeleza programu shirikishi za usafi wa mazingira mijini. Pamoja na mambo mengine, mamlaka zinapaswa kutekeleza Mwongozo wa EWURA wa Usimamizi wa Huduma ya Majitaka na Topekinyesi kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2020;
f) Mamlaka za maji kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa kuandaa utaratibu wa pamoja ambao utafafanua majukumu na wajibu wa mamlaka za maji, halmashauri na wadau wengine katika kuboresha utoaji wa huduma za usafi wa mazingira katika maeneo yao ya huduma;
g) Mamlaka za maji za mikoa kujumuisha katika mipango yao ya biashara mikakati ya matumizi bora ya vyanzo vya maji vilivyopo, ujenzi wa vyanzo vipya vya maji na utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji; na
h) Mamlaka za mikoa na miradi ya kitaifa kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato ya uendeshaji. Hii ni pamoja na kutumia bei sahihi, kuongeza upatikanaji wa huduma na kuongeza ufanisi wa uendeshaji.

Kwa ujumla, hakuna pendekezo lililotolewa katika Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 lililotekelezwa kikamilifu.

### 2.13 Utekelezaji wa Masharti ya Bei za Maji

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kiudhibiti, EWURA hufanya mapitio ya bei za maji kama ambavyo huwasilishwa na mamlaka za maji. Mapitio ya bei hizo huambatana na masharti. Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 11, ambazo ni Arusha, Moshi, Songea, Mtwara, Tabora, Babati, HTM, Igunga, Nzega, Lushoto, na Mbulu zilikua na masharti ya kutekeleza. Aidha, utekelezaji wa masharti ya bei za maji umeimarika na kufikia asilimia 58 ikilinganishwa na asilimia 51 na 48 zilizofikiwa katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2020/21 mtawalia. Hakuna mamlaka ya maji ambayo iliweza kutekeleza kikamilifu masharti ya bei katika mwaka wa fedha 2022/23.

### 2.14 Utekelezaji wa Maagizo ya Ukaguzi

Wakati wa ukaguzi na ufuatiliaji wa ubora wa majisafi na majitaka katika mamlaka za maji, EWURA ilitoa jumla ya maagizo 638 kwa mamlaka hizo kwa ajili ya utekelezaji. Tathmini ya utekelezaji wa maagizo hayo inaonesha kuwa, maagizo 561, sawa na asilimia 88 yalitekelezwa kikamilifu na mamlaka za maji. Ni rai ya EWURA kuwa mamlaka za maji zihakikishe zinatekeleza kikamilifu maagizo ya ukaguzi ili kuboresha utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira nchini.

### 2.15 Hali ya Menejimenti na Watumishi

Katika mwaka wa mapitio, jumla ya watumishi wa mamlaka za maji iliongezeka hadi 6,073 ikilinganishwa na 5,998 katika mwaka wa fedha wa 2021/22 na 5,756 katika mwaka wa fedha 2020/21. Idadi ya watumishi waliokuwepo kwenye mamlaka za maji ilikuwa ni asilimia 91 ya watumishi wanaohitajika. Aidha, idadi ya watumishi wanawake iliongezeka mfululizo na kufikia1,750 katika mwaka wa fedha wa 2022/23 kutoka 1,700 katika mwaka wa fedha 2021/22 na 1,625 katika mwaka wa fedha 2020/21.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 USHINDANISHAJI WA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI

Sehemu hii inawasilisha taratibu zilizotumika kushindanisha mamlaka za maji na matokeo yake kama ifuatavyo:

### 3.1 Taratibu za ushindanishaji

Ushindanishaji wa utendaji wa mamlaka za maji ulifanyika kwa mujibu wa Mwongozo wa EWURA wa Upimaji wa Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2022. Katika mwongozo huo, mamlaka za maji zimegawanywa katika makundi matatu kulingana na idadi ya wateja. Kundi la I ni mamlaka za maji zenye wateja zaidi ya 20,000, Kundi la II ni mamlaka za maji zenye wateja kati ya 5,000 na 20,000, na Kundi la III ni mamlaka za maji zenye wateja chini ya 5,000.

### 3.2 Matokeo ya Ushindanishaji

Kwa kuzingatia vigezo vya ushindanishaji, matokeo ya utendaji wa mamlaka za maji ni kama ifuatavyo:

#### Kundi la I

i. Mamlaka ya Maji ya Iringa iliibuka mamlaka bora kwa ujumla katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 19 za Kundi la I ikiwa na alama 77.7 inayotafsiriwa kama Vizuri sana wakati Mamlaka ya Maji ya Rombo ikiwa na utendaji wa chini zaidi katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa alama 45.8 ambayo ni wastani.
ii. Mamlaka ya Maji ya Tabora iliibuka mamlaka bora katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea katika mpango wake wa biashara wakati mamlaka za maji za Mwanza Kahama na Bukoba zikiwa na utendaji wa chini zaidi ambao hauridhishi.

#### Kundi la II

i. Mamlaka ya Maji ya Nzega iliibuka mamlaka bora kwa ujumla katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 18 za Kundi la II ikiwa na alama 83.3 inayotafsiriwa kama Vizuri sana, wakati Mamlaka ya Maji ya Korogwe ikiwa na utendaji wa chini zaidi katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa alama 37.5 ambayo hairidhishi.
ii. Mamlaka ya Maji ya Lindi iliibuka mamlaka bora katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea katika mpango wake wa biashara wakati mamlaka za maji za Geita, Njombe na Korogwe zikiwa na utendaji wa chini zaidi ambao hauridhishi.

### Kundi la III

i. Mamlaka ya Maji ya Biharamulo iliibuka mamlaka bora kwa ujumla katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 48 za Kundi la III, ikiwa na alama 75.4 inayotafsiriwa kama Vizuri Sana, wakati Mamlaka ya Maji ya Songe ikiwa na utendaji wa chini zaidi katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa alama 30.2, ambayo hairidhishi.

ii. Mamlaka ya Maji ya Mbinga iliibuka mamlaka bora katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea katika mpango wake wa biashara wakati mamlaka za maji za Mugango-Kiabakari, Chato, Chunya, Gairo, Ifakara, Kibaya, Kibondo, Kilindoni, Kilwa Masoko, Kiomboi, Kyela-Kasumulu, Liwale, Ludewa, Mahenge, Namanyere, Namtumbo, Ruangwa, Rujewa, Songe, Tunduru, Ushirombo, Maganzo na Turiani zikiwa na utendaji wa chini zaidi ambao hauridhishi.

Matokeo ya Ushindanishaji wa Mamlaka za Maji kwa makundi yote yameainishwa katika jedwali Na. 4-6 la Taarifa hii.

Ulinganisho wa utendaji wa mamlaka za maji kutoka mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2022/23 ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 3. Kwa ujumla, katika mwaka wa fedha 2022/23 utendaji wa mamlaka za maji umeendelea kuimarika kutokana na kupungua kwa mamlaka za maji zenye utendaji usioridhisha.

**Jedwali Na.3 Ulinganisho wa utendaji wa jumla wa Mamlaka za Maji kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2022/23**

| Mwaka wa Fedha | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|
| Idadi ya Mamlaka Zilizoshindanishwa | 91 | 90 | 85 |
| Utendaji wa Jumla (kwa asilimia) | | | |
| Bora zaidi | 0 | 0 | 0 |
| Vizuri sana | 13 | 17 | 12 |
| Vizuri | 25 | 29 | 27 |
| Wastani | 27 | 31 | 38 |
| Usioridhisha | 26 | 13 | 8 |

**Jedwali Na 4: Matokeo ya Ushindanishaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la I**

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) |
| 1 | Arusha | 38.6 | 19.1 | 57.7 | C | Vizuri | 17 | 63.8 | C | Vizuri | 9 |
| 2 | Dodoma | 41.3 | 22.2 | 63.5 | C | Vizuri | 12 | 63.9 | C | Vizuri | 8 |
| 3 | Iringa | 46.7 | 30.9 | 77.7 | B | Vizuri Sana | 1 | 53.3 | D | Wastani | 15 |
| 4 | Mbeya | 49.0 | 23.7 | 72.7 | B | Vizuri Sana | 4 | 66.8 | C | Vizuri | 4 |
| 5 | Morogoro | 39.9 | 22.0 | 61.9 | C | Vizuri | 16 | 62.4 | C | Vizuri | 10 |
| 6 | Moshi | 45.5 | 31.1 | 76.6 | B | Vizuri Sana | 2 | 66.2 | C | Vizuri | 5 |
| 7 | Musoma | 37.6 | 30.9 | 68.5 | C | Vizuri | 9 | 44.7 | D | Wastani | 16 |
| 8 | Mwanza | 38.7 | 24.3 | 63.0 | C | Vizuri | 15 | 0.0 | E | Usioridhisha | 17 |
| 9 | Shinyanga | 40.0 | 29.9 | 69.9 | C | Vizuri | 8 | 60.9 | C | Vizuri | 11 |
| 10 | Songea | 49.9 | 20.9 | 70.8 | B | Vizuri Sana | 6 | 65.2 | C | Vizuri | 7 |
| 11 | Tabora | 45.5 | 20.6 | 66.2 | C | Vizuri | 11 | 85.9 | A | Bora Zaidi | 1 |
| 12 | Tanga | 45.0 | 29.3 | 74.2 | B | Vizuri Sana | 3 | 66.0 | C | Vizuri | 6 |
| 13 | Bukoba | 38.8 | 24.5 | 63.3 | C | Vizuri | 13 | 0.0 | E | Usioridhisha | 17 |
| 14 | Kigoma | 39.7 | 15.9 | 55.5 | C | Vizuri | 18 | 60.7 | C | Vizuri | 12 |
| 15 | Babati | 41.6 | 28.9 | 70.5 | B | Vizuri Sana | 7 | 74.8 | B | Vizuri Sana | 2 |
| 16 | Kahama | 38.7 | 24.4 | 63.0 | C | Vizuri | 14 | 0.0 | E | Usioridhisha | 17 |
| 17 | DAWASA | 42.8 | 29.4 | 72.2 | B | Vizuri Sana | 5 | 60.3 | C | Vizuri | 13 |
| 18 | KASHWASA | 43.2 | 25.1 | 68.3 | C | Vizuri | 10 | 73.0 | B | Vizuri Sana | 3 |
| 19 | Rombo | 28.6 | 17.2 | 45.8 | D | Wastani | 19 | 58.4 | C | Vizuri | 14 |

**Jedwali Na. 5: Matokeo ya Ushindanishaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la II**

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) |
| 1 | Mtwara | 35.9 | 18.1 | 54.0 | D | Wastani | 10 | 67.9 | C | Vizuri | 3 |
| 2 | Singida | 38.3 | 19.1 | 57.4 | C | Vizuri | 7 | 44.1 | D | Wastani | 13 |
| 3 | Sumbawanga | 39.0 | 15.8 | 54.8 | D | Wastani | 9 | 49.0 | D | Wastani | 11 |
| 4 | Lindi | 35.1 | 21.8 | 56.9 | C | Vizuri | 8 | 84.9 | B | Vizuri Sana | 1 |
| 5 | Geita | 34.3 | 19.2 | 53.5 | D | Wastani | 11 | 0.0 | E | Usioridhisha | 16 |
| 6 | Mpanda | 28.6 | 16.8 | 45.4 | D | Wastani | 15 | 50.0 | D | Wastani | 10 |
| 7 | Njombe | 29.8 | 17.9 | 47.8 | D | Wastani | 14 | 0.0 | E | Usioridhisha | 16 |
| 8 | MANAWASA | 39.5 | 13.7 | 53.1 | D | Wastani | 12 | 65.4 | C | Vizuri | 4 |
| 9 | Wanging'ombe | 24.7 | 16.7 | 41.4 | D | Wastani | 17 | 70.9 | B | Vizuri Sana | 2 |
| 10 | Bunda | 37.6 | 26.8 | 64.4 | C | Vizuri | 4 | 52.3 | D | Wastani | 9 |
| 11 | Igunga | 42.4 | 31.4 | 73.9 | B | Vizuri Sana | 2 | 56.0 | C | Vizuri | 7 |
| 12 | Karatu | 23.8 | 17.6 | 41.4 | D | Wastani | 16 | 43.7 | D | Wastani | 14 |
| 13 | Korogwe | 24.3 | 13.2 | 37.5 | E | Usioridhisha | 18 | 0.0 | E | Usioridhisha | 16 |
| 14 | Nzega | 46.3 | 37.0 | 83.3 | B | Vizuri Sana | 1 | 53.9 | D | Wastani | 8 |
| 15 | Sengerema | 39.9 | 19.5 | 59.4 | C | Vizuri | 6 | 45.5 | D | Wastani | 12 |
| 16 | Tukuyu | 31.6 | 21.0 | 52.6 | D | Wastani | 13 | 62.0 | C | Vizuri | 6 |
| 17 | Makambako | 38.2 | 23.4 | 61.5 | C | Vizuri | 5 | 65.3 | C | Vizuri | 5 |
| 18 | Busega | 40.0 | 30.5 | 70.5 | B | Vizuri Sana | 3 | 40.0 | D | Wastani | 15 |

**Jedwali Na. 6: Matokeo ya Ushindanishaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la III**

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) |
| 1 | Bariadi | 33.4 | 27.0 | 60.3 | C | Vizuri | 9 | 61.1 | C | Vizuri | 12 |
| 2 | Vwawa-Mlowo | 29.9 | 17.0 | 46.9 | D | Wastani | 28 | 47.6 | D | Wastani | 20 |
| 3 | Makonde | 33.4 | 27.1 | 60.5 | C | Vizuri | 8 | 56.2 | C | Vizuri | 16 |
| 4 | HTM | 29.9 | 17.7 | 47.6 | D | Wastani | 25 | 56.8 | C | Vizuri | 15 |
| 5 | Mugango-Kiabakari | 29.3 | 13.6 | 42.9 | D | Wastani | 37 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 6 | Maswa | 39.8 | 27.1 | 66.9 | C | Vizuri | 2 | 62.2 | C | Vizuri | 11 |
| 7 | Biharamulo | 44.0 | 31.4 | 75.4 | B | Vizuri Sana | 1 | 82.6 | B | Vizuri Sana | 2 |
| 8 | Chato | 35.5 | 14.2 | 49.6 | D | Wastani | 22 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 9 | Chunya | 30.1 | 13.0 | 43.2 | D | Wastani | 35 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 10 | Gairo | 30.3 | 16.0 | 46.3 | D | Wastani | 29 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 11 | Ifakara | 25.2 | 13.7 | 38.8 | E | Usioridhisha | 44 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 12 | Itumba-Isongole | 31.6 | 21.0 | 52.6 | D | Wastani | 19 | 43.9 | D | Wastani | 23 |
| 13 | Kasulu | 34.5 | 17.4 | 51.9 | D | Wastani | 21 | 48.0 | D | Wastani | 19 |
| 14 | Kibaya | 29.7 | 13.4 | 43.1 | D | Wastani | 36 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 15 | Kibondo | 28.2 | 16.3 | 44.5 | D | Wastani | 32 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 16 | Kilindoni | 17.3 | 13.2 | 30.4 | E | Usioridhisha | 47 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 17 | Kilwa Masoko | 29.5 | 11.1 | 40.6 | D | Wastani | 41 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) |
| 18 | Kiomboi | 32.8 | 14.2 | 47.0 | D | Wastani | 27 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 19 | Kishapu | 38.7 | 23.8 | 62.6 | C | Vizuri | 7 | 64.8 | C | Vizuri | 8 |
| 20 | Kondoa | 34.4 | 18.3 | 52.7 | D | Wastani | 17 | 46.1 | D | Wastani | 22 |
| 21 | Kyela-Kasumulu | 28.0 | 11.1 | 39.0 | E | Usioridhisha | 43 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 22 | Liwale | 28.4 | 14.4 | 42.8 | D | Wastani | 38 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 23 | Loliondo | 40.2 | 25.6 | 65.8 | C | Vizuri | 3 | 70.5 | B | Vizuri Sana | 5 |
| 24 | Ludewa | 24.7 | 15.8 | 40.6 | D | Wastani | 42 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 25 | Lushoto | 35.1 | 18.3 | 53.4 | D | Wastani | 16 | 62.9 | C | Vizuri | 10 |
| 26 | Mafinga | 39.6 | 20.5 | 60.1 | C | Vizuri | 11 | 64.9 | C | Vizuri | 7 |
| 27 | Mahenge | 26.1 | 15.0 | 41.1 | D | Wastani | 40 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 28 | Makete | 30.7 | 16.8 | 47.5 | D | Wastani | 26 | 53.7 | D | Wastani | 17 |
| 29 | Manyoni | 41.2 | 21.9 | 63.1 | C | Vizuri | 6 | 66.0 | C | Vizuri | 6 |
| 30 | Mbinga | 41.0 | 19.1 | 60.1 | C | Vizuri | 10 | 85.9 | A | Bora Zaidi | 1 |
| 31 | Mbulu | 36.5 | 18.3 | 54.8 | D | Wastani | 14 | 64.6 | C | Vizuri | 9 |
| 32 | Mpwapwa | 36.9 | 18.9 | 55.9 | C | Vizuri | 13 | 60.4 | C | Vizuri | 13 |
| 33 | Mwanhuzi | 30.2 | 15.0 | 45.1 | D | Wastani | 30 | 22.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 34 | Namanyere | 21.0 | 11.4 | 32.5 | E | Usioridhisha | 46 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 35 | Namtumbo | 31.3 | 12.0 | 43.2 | D | Wastani | 34 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 36 | Ngara | 35.5 | 28.3 | 63.8 | C | Vizuri | 5 | 57.6 | C | Vizuri | 14 |
| 37 | Orkesumet | 41.9 | 23.8 | 65.7 | C | Vizuri | 4 | 76.6 | B | Vizuri Sana | 4 |

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishaji wa Jumla | | | | Ushindanishaji kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2022/23) |
| 38 | Ruangwa | 28.0 | 14.0 | 42.0 | D | Wastani | 39 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 39 | Rujewa | 25.0 | 18.4 | 43.4 | D | Wastani | 33 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 40 | Same-Mwanga | 31.3 | 18.2 | 49.4 | D | Wastani | 24 | 47.6 | D | Wastani | 21 |
| 41 | Songe | 16.7 | 13.6 | 30.2 | E | Usioridhisha | 48 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 42 | Tunduru | 23.9 | 12.0 | 35.9 | E | Usioridhisha | 45 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 43 | Ushirombo | 35.8 | 13.8 | 49.6 | D | Wastani | 23 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 44 | Utete | 35.3 | 23.9 | 59.3 | C | Vizuri | 12 | 52.0 | D | Wastani | 18 |
| 45 | Maganzo | 37.5 | 14.9 | 52.5 | D | Wastani | 20 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |
| 46 | Mombo | 26.0 | 19.1 | 45.1 | D | Wastani | 31 | 43.4 | D | Wastani | 24 |
| 47 | Tunduma | 33.2 | 20.9 | 54.1 | D | Wastani | 15 | 77.0 | B | Vizuri Sana | 3 |
| 48 | Turiani | 36.5 | 16.2 | 52.6 | D | Wastani | 18 | 0.0 | E | Usioridhisha | 26 |

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 MASUALA YALIYOBAINIKA NA MAPENDEKEZO

Sehemu hii inaorodhesha masuala muhimu yaliyobainika katika Taarifa ya Utendaji wa mamlaka za maji kwa mwaka wa fedha 2022/23 ambayo yanahitaji kuboreshwa. Inatarajiwa kwamba, endapo mamlaka za maji zitatekeleza kikamilifu mapendekezo yaliyoainishwa katika taarifa hii, huduma ya majisafi na usafi wa mazingira itazidi kuimarika.

**Jedwali Na. 7: Masuala Yaliyobainika na Mapendekezo**

| Na | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya Mwisho ya Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| i. | Kutokidhi kiwango cha dawa *(residual chlorine levels)* | Mwaka 2022/23, wastani wa kukidhi kiwango cha dawa (*residual chlorine level*) kilikuwa ni asilimia 84. Kiwango hicho hakikidhi na kipo chini ya kiwango kinachotakiwa cha asilimia 100 | Mamlaka za Maji ziboreshe kukidhi viwango vya dawa *(residual chlorine)* kwa:-<br>(i) kuandaa na kuwa na vituo/sehemu vya kupima na kufuatilia viwango vya dawa kabla maji hayaja sambazwa;<br>(ii) kutukmia kifaa ambacho kimefanyiwa uhakiki sahihi wa upimaji wa kiwango cha dawa (residual chlorine); na<br>(iii) kuhakikisha kwamba shughuli za utibuji wa maji zinafanywa na mtaalam wa dawa | Juni 2025 | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |
| ii. | Majitaka yaliyotibiwa kutokidhi viwango vya ubora kwenye viashiria vya mahitaji ya oksijeni kibiolojia na kikemikali (BOD na COD); | Mwaka 2022/23, viwango vya ubora vya majitaka yaliyotibiwa kwenye viashiria vya mahitaji ya oksijeni kibaiolojia na kikemikali (BOD na COD) vilikuwa asilimia 58 and 50, mtawalia. Viwango hivyo havijafikia viwangongo vinavyohitajika vya asilimia 100 | (i) Mamlaka za maji zinapaswa kujenga miundombinu ya kutibu majitaka na kuongeza uwezo wa miundombinu iliyopo ya kutibu majitaka ili kukidhi mahitaji; na<br>(ii) Mamlaka za maji zinapaswa kukarabati miundombinu ya kutibu majitaka | Juni 2026 | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |

| Na | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya Mwisho ya Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| iii. | Uwiano mdogo wa idadi ya watu wanaopata huduma ya majisafi na usafi wa mazingira | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya majisafi katika maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya maji ni asilimia 82. Kiwango hiki bado hakijafikia lengo la asilimia 95 kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maenedeleo kwa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) | Mamlaka za maji ziandae mipango ya biashara ambayo itakuwa imejumuisha mikakati ya kufikia asilimia 95 ya utoaji huduma ya maji. Mikakati hiyo ihusishe upatikanaji wa fedha za uwezekezaji kupitia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (*Public Private Partinership).* Pia, mamlaka za maji zichukue hatua mahsusi za kuongeza upatikanaji wa huduma za maji | Juni 2025 | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |
| iv. | Upotevu mkubwa wa maji wa zaidi ya asilimia 20 inayokubalika | Kwa mwaka 2022/23 kiwango cha upotevu wa maji kilikuwa asilimia 37, kiwango hicho ni kikubwa kuliko kiwango kinachokubalika kisichozidi asilimia 20 | (i) Mamlaka za maji zichukue hatua stahiki za kuhakikisha upotevu wa maji hauzidi kiwango kinachokubalika cha chini ya asilimia 20. Hatua hizo ni pamoja na kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa maji kwa mujibu wa Mwongozo wa EWURA wa Kuandaa Mkakati wa Kupunguza Upotevu wa Maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021 | Juni 2024 | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |
| | | | (ii) Mamlaka za maji kuhakikisha zinatekeleza Mikakati ya Kupunguza Upotevu wa Maji katika mamlaka zao za maji | Endelevu | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |

| Na | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya Mwisho ya Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| v. | Uchache wa miundombinu ya miundombinu ya kutibu majitaka na topetaka kinyesi | Mamlaka 64 kati ya 85 hazina miundombinu ya kutibu majitaka na topetaka kinyesi. Hii inaashiria kuna hatari ya afya na mazingira | (i)Mamlaka za maji zijumuishe kwenye Mipango Biashara yao mikakati ya kupata ardhi/eneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topetaka kinyesi | Juni 2025 | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |
| | | | Wizara ya Maji inashauriwa kuzisaidia mamlaka za maji fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka na topetaka kinyesi.<br><br>Pia, ushirikishwaji wa sekta binafsi unaweza ukaangaliwa kama njia mbadala | Juni 2026 | Wizara ya Maji |
| vi. | Uwiano mdogo wa uzalishaji wa maji ikilinganishwa na mahitaji | Licha ya uwepo wa miundombinu yenye uwezo wa kutosha wa kuzalisha maji, kiwango cha maji yanayozalishwa na baadhi ya mamlaka za maji bado kimeenedelea kutokidhi mahitaji | Mamlaka za maji zihakikishe zinatumia kikamilifu uwezo wa miundombinu ya uzalishaji maji iliyopo ikiwa ni pamoja na kuongeza mtandao wa usambazaji maji ili kuendana na ongezeko la wateja | Juni 2025 | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |
| vii. | Bei za maji za muda mrefu ambazo haziendani na gharama halisi za uendeshaji | Baadhi ya mamlaka za maji kuendelea kutumia bei za maji kwa muda mrefu ambazo haziendani na gharama halisi za uendeshaji na uwekezaji | (i)Mamlaka za maji ziandae mipango ya biashara ili pamoja na mambo mengine ziweze kubaini gharama halisi za utoaji huduma na kufanya marekebisho ya bei | June 2025 | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |
| | | | (ii) Wizara ya Maji inashauriwa kuzisaidia Mamlaka za maji kuwa na wataalam wa kutosha kulingana na muundo wa mamlaka za maji uliopitishwa | Juni 2025 | Wizara ya Maji |

| Na | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya Mwisho ya Utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| viii. | Upatikani wa huduma isiyotesheleza ya usafi wa mazingira | Katika mwaka 2022/23, watu wanaopata huduma ya usafi wa mazingira kutoka kwenye miundombinu ya majitaka ni asilimia 11. Kiwango hiki bado kipo chini ya asilimia 100 ambayo inakubalika. Pia, mamlaka 21 kati ya 85 zina miundombinu ya kutibu majitaka na topetaka kinyesi. | (i) Mamlaka za maji kubuni na kutekeleza programu shirikishi za usafi wa mazingira mijini *(City Wide Inclusive Sanitation Approach)*<br><br>(ii) Mamlaka za maji zinapaswa kutekeleza Mwongozo wa EWURA wa Usimamizi wa Huduma ya Majitaka na Topekinyesi kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2020 | Endelevu | Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira |

EWURA Makao Makuu
Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA,
41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 26 2 329 002-4 • Nukushi: +255 26 2329005
www.ewura.go.tz

ewuratanzania ewuratv

Simu ya Bure: 0800110030

Piga *152*00# Kufahamu Bei ya Mafuta

PERUZI HAPA